# SPEAR SERIES

# STD 6 - TERM III

# KISWAHILI

**Jaza nafasi zilizo wazi**

Ajira __1__ watoto ni jambo __2___ linastahili kupigwa na kila __3__ wetu. Ingawa sheria zimepitishwa kuhusu hatua zifaazo kuchukuliwa . __4___ ya wale wanaodhulumu watoto. Baadhi ya matajiri __5___ sheria hii. Bado kuna watoto fulani wanaajiriwa kuwa vijakazi na __6__ katika mashamba ya mabwenyenywe hao.

Kila mtoto ana haki ya kupata __7___, hasa wakati huu ambao __8___ imeanzisha elimu bila malipo katika shule za msingi. Vile vile watoto wana haki ya kupata lishe __9___, kutibiwa wanapo ___10__, kuishi katika mazingira __11__, kuvishwa mavazi ya kuwasetiri __12__ na pia kupewa ___13___ ya kucheza na __14__ Je, wewe mwanafunzi una haki hizi __15___.


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. wa | B. cha | C. ya | D. la |
| 2. | A. ambao | B. ambalo | C. ambayo | D. ambacho |
| 3. | A. mmoja | B. moja | C. mumoja | D. mmocha |
| 4. | A. na | B. kwa | C. katika | D. dhidi |
| 5. | A. wanakiuka | B. yanakiuka | C. yanayokiuka | D. wanaokiuka |
| 6. | A. vibarua | B. vijikazi | C. wakazi | D. waakazi |
| 7. | A. elimu | B. kielimu | C. ilimu | D. maelimu |
| 8. | A. serekali | B. sirikali | C. serikali | D. serikari |
| 9. | A. mbora | B. bora | C. bola | D. mbola |
| 10. | A. gonjeka | B. ungua | C. gonjwa | D. ugua |
| 11. | A. masafi | B. safi | C. misafi | D. msafi |
| 12. | A. uchi | B. uji | C. unji | D. nje |
| 13. | A. furza | B. fulsa | C. fursa | D. fusa |
| 14. | A. wenzangu | B. wenzake | C. wenzao | D. mwenzangu |
| 15. | A. , | B. . | C. ! | D. ? |

**Chagua jibu sahihi kujaza pengo**

16. Ziara yetu ilianza saa 12:45 asubuhi. Hii ni saa
    - A. sita kasorobo
    - B. moja kasorobo
    - C. saba kasorobo
    - D. kumi na mbili kasorobo
17. Uchafu wa machoni ni matongo. Uchafu wa meno ni
    - A. kigaga
    - B. masizi
    - C. usaha
    - D. utaya
18. Kulalia kifua ni kulala ________
    - A. kingalingali
    - B. chali
    - C. kifudifudi
    - D. kifundifundi
19. Eleza maana ya msemo: Kutia nanga.
    - A. Kuanza safari
    - B. Kuongeza chumvi katika mambo
    - C. Kuacha safari
    - D. Kufika mwisho wa jambo hasa safari
20. **Kitendawili:** Nikiita anaita. Nikiitika anaitika ____
    - A. boga
    - B. mwangwi
    - C. sauti
    - D. mtoto

21. **Tegua jibu sahihi.**

Taja maumbo haya mtawalia.



A. wima, moyo　　B. msitari sulubu, roho

C. pembe kuu, kopa　　D. mstari sulubu, kopa

**<u>Andika kwa wingi</u>**

22. Kufuli hufunga mlango.

A. Vifuli hufunga milango

B. Vifuli huyafunga malango

C. Makufuli huifunga milango

D. Makufuli huyafunga malango

23. Nomino Kengele hupatikana katika ngeli ipi?

A. ki - vi　　B. li - ya

C. i - zi　　D. u - zi

24. Akisami $^1/_7$ huitwa ________

A. sudusi　　B. subui

C. tusui　　D. thumuni

25. Chagua sentensi iliyoandikwa sawa kisarufi.

A. Nilikuwa nikienda shuleni nilioanguka

B. Mimi ndiye niliyekuwa mshindi

C. Maskani mwangu mna raha tele

D. Utosini pangu pana mvi

**<u>Jibu maswali yafuatayo kulingana na maagizo</u>**

26. Maswali tuliyoulizwa ni <u>mboga.</u> Kwa hivyo ni _____

A. magumu　　B. yanatatiza

C. rahisi　　D. yana makosa mengi

27. Makooni pa kuku, utawapata wadudu wapi?

A. Utiriri　　B. Tekenya

C. Kunguni　　D. Ruba

28. Nyumbani ______ pana maji mazuri.

A. petu　　B. kwetu

C. mwetu　　D. yetu

29. **<u>Chagua tashbihi inayofaa kukamilisha sentensi ifuatayo.</u>**

Msichana huyu ni misi kama _________

A. ufizi　　B. taya

C. gego　　D. choge

30. Andika kwa maneno.30,002

A. Elfu thelathini na mbili

B. Elfu thelathini na mbili na mbili

C. Thelathini na mbili elfu

D. Thelathini elfu na mbili

**<u>Soma habari hii kisha ujibu maswali 31-40</u>**

Katika miaka ya hivi karibuni kumeshuhudiwa mabadiliko makubwa ya kijamii katika taifa letu. Miongoni mwa mabadiliko hayo ni kuendelea kwa taifa kuwa changa. Hii ina maana kuwa wananchi vijana ni walio na miaka chini ya thelathini na mitano iliyopita. Mbinu za kujua kusoma na kuandika huchukuliwa kuwa kitu cha kawaida kama vile kuvaa nguo.

Tukitupa macho nyuma kabla ya utawala wa kikoloni kuingia huku kwetu yapata karne moja iliyopita tutaona kuwa hali ilikuwa tofauti kabla jumuiya zilizoishi katika sehemu ya bara hazikuwa zimeona wala kusikia mtu akiandika ama kusoma. Angetokea mtu awasomee makala wangemwona kama mwehu anayeboboka ovyo kwani hicho kilikuwa kioja kikubwa.

Jumuiya za pwani zilikuwa na hali tofauti karne kadhaa hapo awali. Wananchi hawa walikuwa wametembelewa na waarabu kwa njiti la kufaanya biashara na kuwachubilia dini ya Kiisilamu. Maingiliano haya yaliwanufaidha wananchi kwa njia ambayo labda haikukusudiwa. Walipata ujuzi wa kusoma na kuandika hati ya kiarabu ili waweze kusoma Koran kwa lugha ya Kiarabu. Baadaye walitumia hati hiyo kuandika lugha zao za kienyeji. Maandishi mengi yalikuwa na lengo la kuhifadhi mafunzo ya dini ya kiisilamu.

Tukizingatia wazo hili na kulichunguza baadhi ya jumuiya zilizoishi bara tutaona kuwa zilikuwa na aina ya uandishi. Katika jumuiya mojawapo kwa mfano, mgeni aliposema angekuja kutembea baada ya siku kumi, wenyeji wake walichukua ukamba wakatengeneza mafundo kumi. Kila ufundo uliwakilisha siku moja. Kila kulipokucha waliondoa

fundo moja mpaka fundo la kumi. Hii ilikuwa njia mahsusi ya kuhifadhi habari na ililingana na ile ya kuandika.

Tunaweza kusema kuwa ikiwa wakoloni hawakuja na mafumbo mpya, labda kufikia sasa Jumuiya hiyo ingekuwa imevumbua njia nyingine ya uandishi.

31. Kwa nini taifa letu linasemekana kuwa changa?
    A. Kwa sababu lilipata uhuru hivi juzi
    B. Ni taifa ambalo si kubwa sana
    C. Idadi kubwa ya wananchi ni vijana
    D. Halikui kimaendeleo kama nchi zingine

32. Neno jingine lenye maana sawa na <u>mbinu</u> kama lilivyotumiwa kwenye taarifa ni ________
    A. mafunzo B. hati
    C. stadi D. wazo

33. Kulingana na taarifa hii ________
    A. watu wote walijua kuandika kuanzia zamani
    B. wakoloni ndio walikuwa wa kwanza kuwafunza watu kuandika
    C. Siku hizi kusoma na kuandika ni kitu cha kawaida
    D. Waarabu walikuja kutawala sehemu za pwani

34. Waarabu walitaka watu wajue kuandika ________
    A. ili wapate elimu ya juu
    B. ili iwe rahisi kwao kuwatawala
    C. ili waweze kuendeleza dini yao
    D. ili wafanye biashara vyema

35. Watu wa pwani walijua kuandika ________
    A. karibu miaka mia moja iliyopita
    B. miaka zaidi ya mia mbili iliyopita
    C. miaka hamsini iliyopita
    D. mkoloni alipowasili

36. Maana ya neno <u>kioja</u> ni ________
    A. wendawazimu B. ajabu
    C. ghasia D. maarifa

37. Chagua kifungo kilicho sahihi.
    Wenyeji wa pwani walitumia hati ya kiarabu
    A. Kusomea na kuandika korani na lugha zao
    B. Kusomea na kuandika kiarabu na lugha zao
    C. Kusomea na kuandika kiarabu
    D. Kusomea na kuandika kiswahili

38. Wananchi wengi wanajua kusoma na kuandika kwa sababu ________
    A. wananchi wenyewe wamefanya bidii
    B. kumekuwa utulivu nchini
    C. kumekuwa na mpango uliotekelezwa kwa miaka mingi iliyopita
    D. wananchi wanaona faida ya kujua kusoma na kuandika

39. Kabla ya watu kujua kusoma na kuandika
    A. walikuwa hawajui chochote kuhusu idadi
    B. walikuwa na binu zao za kujua idadi
    C. walishindwa kuwasilisha ujumbe
    D. walichukia elimu ya kuhesabu

40. Habari hii inazungumza kuhusu ________
    A. waarabu B. waislamu
    C. wakoloni D. uandishi

**<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50</u>**

Kuna visa vingi vya mikasa ambavyo vimekuwa vikiadhiri maisha ya binadamu hapa duniani. Kati ya mikasa hiyo ni ugaidi, ajali kupitia vyombo vya usafiri hususan magari na ndege, vita, mitetemeko ya ardhi, ukame na mioto.

Katika matukio na maafa ya mikasa hii, nchi yetu haikupona. Haikuachwa nyuma. Vita vya baada ya uchaguzi wa mwaka wa elfu mbili na saba, haujatutoka akilini wala moyoni. Uhasama uliochochewa na vingozi wetu ulitufanya tuuane, tuharibiane mali na zaidi ya yote tuvuruge amani iliyotuongoza kwa zaidi ya miongo mitano.

Hakuna atakayekisahau kitendo kilichofanywa na magaidi walioshambulia ubalozi wa Marekani jijini Nairobi. Katika shabulishi hilo, wakenya zaidi ya mia mbili walipoteza maisha yao. Sisemi maelfu zaidi walio lemezwa na mali ya thamani ya mamilioni kuharibiwa.

Lakini kati ya ajali zote zilizowahi kutokea nchini mwetu katika miaka ya hivi karibuni ni pamoja na mikasa mibaya sana ya moto. Ule mkasa wa duka kuu ya Nakumatt uliwaacha wengi wameachama na kushangaa. Kulingana na habari ambazo hazikuthibitishwa wakurugenzi wa duka hilo waliwaamuru mabawabu kufunga milango pindi waliposikia

mlipuko. Hivyo basi waliwanyima wahasiriwa wa mkasa huo nafasi ya kujiokoa. Inahofiwa kuwa zaidi ya wakenya hamsini huenda walipoteza maisha yao humo: wateja, wapitanjia na wahudumu wa duka hilo hasara iliyoje?

Kabla ya wingu la hofu kutoka, baada ya siku mbili tu, mkasa mwingine wa moto ukalikumba eneo la Shachang'an katika wilaya ya Molo. Kulingana na watu walioshuhudia mkosi huo, trela la mafuta likosa mwerekeo na kupinduka. Hapo wenyeji wakanjua wamepata mavuno. Katika harakati zao za kufyonza na kuteka mafuta trela likalipuka! Ndimi za moto huo wa mafuta zilienea zaidi ya kilomita tano: hata kuwapata wahasiliwa walio katika nyumba zao wote waliokuwa katika eneo hilo la mkasa waliangamia. Kulingana na takwimu zilizotolewa na idara ya polisi watu zaidi ya mia moja na kumi walipoteza maisha yao bila kusahau mamia ya manusura na majeruhi.

Majeruhi waliokuwa katika hali mahututi walisafirishwa na ndege hadi Nairobi kwa matibabu maalum. Wengine walilazwa katika hospitali za Molo na mji wa Nakuru. Swali linaloduru katika akili za kila mkenya ni je, serikali pamoja na mabaraza ya miji yana uwezo kukabiliana na majanga haya? Iwapo mkasa kama huo utazuka tena utakabiliwa vipi?

41. Ni aina gani ya mkasa ambayo haikutajwa kumwathiri sana binadamu?
A. Vita B. Ugaidi
C. Ajali za ndege D. Mafuriko

42. Wananchi walichochewa na kina nani kupigana baada ya uchaguzi mkuu?
A. Wenyewe kwa wenyewe
B. Viongozi
C. Uhasama
D. Ugomvi

43. Shambulizi la kigaidi, lililotajwa lilitenga sehemu gani?
A. Balozi la Kenya nchini Marekani
B. Jengo la Bunge
C. Wizara ya ubalozi
D. Ubalozi wa Marekani hapa nchini

44. Ni katika mkasa gani ambapo ilisemekana kuwa mabawabu walifunga milango?
A. Mkasa wa ndege ya Kenya Airways
B. Mkasa wa trela wa Molo
C. Mkasa wa duka kuu la Nakumatt
D. Mkasa wa vita vya uchaguzi

45. Kitu gani kilisababisha ajali ya moto huko Molo?
A. Trela la mafuta lilipolipuka
B. Watu kufyonza na kuzoa mafuta
C. Trela kugongana na basi
D. Ndimi za moto kufika mbali

46. Mwandishi anaposema nchi yetu haikupona anamaanisha nini?
A. Nchi yetu imepatwa na magonjwa mabaya
B. Nchi yetu haikunusurika kupatwa na majanga
C. Nchi yetu haina madawa za kuponya magonjwa
D. Nchi yetu ina hali mbaya ya umaskini

47. Mwandishi anapotaja kuwa tumeivuruga amani tuliyokuwa nayo kwa zaidi ya miaka mitano inamaanisha nini?
A. Vita viliharibu hali ya amani ya zaidi ya miaka hamsini
B. Tulivuruga amani tuliyokuwa nayo kwa miaka mitano
C. Watu karibu hamsini walikufa vitani
D. Vita huvuruga amani baada ya siku tano

48. Mwandishi amezungumzia visa vingapi vya Molo?
A. Vitano B. Vinne
C. Viwili D. Vingi

49. Swali gani ambalo kila mkenya anajiuliza
A. Ni kwa nini watu wakafungiwa wakafia motoni?
B. Kwa nini serikali haikabiliani na visa vya moto?
C. Mbona visa vya moto vimeongezeka?
D. Iwapo serikali na mabaraza ya miji yana uwezekano wa kukabiliana na visa vya moto?

50. Kichwa mufti kwa taarifa hii ni ________
A. Mikasa mbalimbali B. Mikasa ya moto
C. Trela lililowaka moto D. Sambulizi la kigaidi